TANGAZO LA SERIKALI NA. 510 la tarehe 21/05/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni, gulioni au mnadani kwa lengo la kuuzwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro;

"kodi ya pango" maana yake ni kodi ya pango itakayolipwa na mtu yeyote, chama, taasisi au

shirika lililopanga katika kibanda cha biashara, meza za soko, eneo au jengo lolote la Halmashauri;

"leseni ya biashara" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, kampuni au taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri;

"machinjio" maana yake ni eneo rasmi la kuchinjia wanyama ambalo linamilikiwa na Halmashauri au sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mwalo" maana yake ni chumba cha barafu au jengo lolote lenye vitendanishi vya kuhifadhia samaki na rasilimali zingine za bahari, maziwa, mito na mabwawa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya wananchi kuuzia au kununua bidhaa;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria, bidhaa au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na

Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu mwenye wajibu wa kulipa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii atapaswa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa ukusanyaji wa ada au ushuru

6.-(1) Ada au ushuru utakusanywa kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano kati ya Halmashauri na mlipaji.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukodishaji wa mali na rasilimali za Halmashauri

7. Halmashauri inaweza kupangisha au kukodisha mali na rasilimali zake na kutoza kodi katika majengo, nyumba na vibanda vya biashara au viwanja au maeneo ya biashara na mitambo inayomilikiwa na Halmashauri.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

8.-(1) Ada au ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Mlipa ada au ushuru atakuwa na wajibu wa

kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa siyo utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

9.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu mwenye wajibu wa kulipa atashindwa kulipa ada au ushuru ndani ya muda uliobainishwa.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Endapo mdaiwa atashindwa kulipa deni la ada au tozo ndani ya siku thelathini tangu kukamatwa kwa mali kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), Halmashauri, baada ya kupata idhini ya mahakama, inaweza kuuza mali hizo kwa njia ya mnada.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itaziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya mahakama.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni hii, kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

10.-(1) Halmashauri inaweza kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kuwa wakala wa kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni

ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(3) Wakala atahakikisha malipo ya ushuru yanafanyika kwa njia ya kielektroniki na risiti zinatolewa kwa kila muamala.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

12.-(1) Mtu anatenda kosa endapo-

(a) anashindwa, anadharau, anakwepa au anakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) anamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) anamzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) anatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) anatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya

Halmashauri; au

(f) anatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

13. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibikaa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji wa makosa

14. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kulipa kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

USHURU WA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Mali | Kiwango cha ushuru/Kodi kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko |
| 2. | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko |
| 3. | Kukodi viti | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko |
| 4. | Kukodi Gari: Magari madogo<br>Magari makubwa | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko |
| 5. | Mitambo (Trekta, Vifaa vya GPS Na kadhalika) | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Vibanda na Vizimba vya biashara | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 7. | Kiwanda cha Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 8. | Mwalo | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 9. | Machinjio | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 10. | Viwanja vya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 11. | Matumizi ya choo cha kulipia | | |
| | (a) Kuoga | 500 | |
| | (b) Kujisaidia/Haja | 300 | |
| 12. | Vifaa vya upimaji wa ardhi | Kwa mujibu wa mkataba na bei ya soko | |
| 13. | Maturubai | 3,000 kila moja kwa siku | |
| 14. | Majukwaa ya Halmashauri | 10,000 | |
| 15. | Mahema ya Halmashauri | 10,000 kila moja kwa siku | |
| 16. | Kuogesha mifugo kwenye majosho ya Halmashauri | 500 kila Ng'ombe<br>300 kila Mbuzi/Kondoo<br>200 kila mfugo kwa mifugo mingine | |
| 17. | Ushuru wa kulaza Magari na Pikipiki kwenye yadi ya Halmashauri | 1,000 | Kila Gari kwa siku |
| | | 500 | Kila Pikipiki au chombo cha Magurudumu matatu |

SEHEMU YA PILI

ADA NA USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiasi (Shilingi) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Machinjio: Ng'ombe | 5,000 | Kwa ng'ombe mmoja atakayechinjwa |
| 2. | Ushuru wa Machinjio: Kondoo na Mbuzi | 1,000 | Kwa kondoo mmoja atakayechinjwa |
| | Ushuru wa machinjio: Nguruwe | 1,500 | Kwa nguruwe mmoja atakayechinjwa |
| 3. | Ushuru wa Machinjio: Jamii ya ndege | 200 | Kwa mmoja atakayechinjwa |

*Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Ada ya Ukaguzi: Ng'ombe | 2,000 | Kwa ngo'mbe mmoja atakayechinjwa |
| 5. | Ada ya Ukaguzi: Kondoo, Mbuzi na Nguruwe | 1,000 | Kila mmoja atakayechinjwa |
| 6. | Ada ya ukaguzi: Kuku na jamii ya ndege | 200 | Kila mmoja atakayechinjwa |
| 7. | Ukaguzi wa Bucha | 500 | Kwa siku ya ukaguzi |

SEHEMU YA TATU
USHURU WA MADINI YA UJENZI

| *Namba* | *Aina ya chanzo* | *Kiwango cha Ada au ushuru (Shilingi)* | *Kiasi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya kibali cha kuchimba Mchanga, Udongo, Kifusi au madini mengine | 200,000 | Kila kibali (Tani 1,000). |
| 2. | Ada ya kibali cha kuchimba Mawe | 150,000 | Kila kibali |
| 3. | Ushuru wa kusafirisha, Udongo, Mchanga au Kifusi | 1,500 | Tani moja |
| 4. | Ushuru wa kusafirisha Kokoto, Tarazo, Changarawe au Mawe ya kujengea | 2,000 | Tani moja |
| 5. | Ushuru wa kusafirisha Chokaa | 1,000 | Tani moja |
| 6. | Ushuru wa kusafirisha Madini mengine | 1,500 | Tani moja |

SEHEMU YA NNE
ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kibali cha ngoma za jadi | 10,000 | Kwa tukio |
| 2. | Kibali cha kuchezesha Disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za Maonyesho, Sinema na Matamasha | 15,000 | Kwa kibali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha | 10,000 | Kwa kibali |
| 4. | Kibali cha Mechi kuendesha mashindano ya Mipira | 30,000 | Kwa kibali |
| 5. | Kibali cha kuchezesha disco usiku (Night club) | 60,000 | Kwa kibali |
| 6. | Tiba za jadi | 10,000 | Kwa mwaka |
| 7. | Kuendesha promotion kwenye baa, hoteli viwanja vya wazi | 20,000 | Kwa siku |
| 8. | Ada za shughuli za jando na unyago | 20,000 | Kwa tukio |
| 9. | Kuchezesha pool table | 5,000 | Kwa kila meza kwa mwaka |
| 10. | Usajili wa vikundi vya ngoma | 30,000 | Kwa mwaka |
| 11. | Banda la video | 30,000 | Kwa mwaka |
| 12/ | Ada ya Kibali cha waganga wa Jadi | 20,000 | Kwa miezi sita (6) |

## SEHEMU YA TANO
## USHURU WA MASHAMBA MAKUBWA, UKAGUZI WA RAMANI NA VIBALI VYA UJENZI

*Ada za ukaguzi wa ramani na vibali vya ujenzi/Ukarabati wa Jengo/ubomoaji wa Jengo*

| *Namba* | *Kibali cha ujenzi* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Jengo la makazi | 70,000 | kwa kibali |
| 2. | Jengo la makazi ghorofa moja | 50,000 | kwa kibali |
| 3. | Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja | 100,000 | kwa kibali |
| 4. | Jengo la makazi na biashara | 150,000 | kwa kibali |
| 5. | Nyumba za biashara (Guest house& Hotel) | 100,000 | kwa kibali |
| 6. | Jengo la biashara | 180,000 | kwa kibali |
| 7. | Jengo la biashara ghorofa moja | 200,000 | kwa kibali |
| 8. | Jengo la biashara zaidi ya ghorofa moja | 250,000 | kwa kibali |
| 9. | Jengo la kiwanda | 100,000 | kwa kibali |
| 10. | Jengo la taasisi | 500,000 | kwa kibali |
| 11. | Vibanda vya biashara | 50,000 | kwa kibali |
| 12. | Ujenzi wa uzio wa kudumu | 1,000 | kwa mita kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kila kibali |
| 13. | Ujenzi wa uzio wa muda | 500 | kwa mita kwa kila kibali |
| 14. | Kukata barabara | 25,000 | kwa mita kwa kila kibali |
| 15. | Minara ya simu | 300,000 | kwa kibali |
| 16. | Kituo cha Mafuta | 250,000 | kwa kibali |
| 17. | Ofisi, Shule, Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali binafsi | 100,000 | kwa kibali |
| 18. | Maghala na Bohari | 200,000 | kwa kibali |
| 19. | Ukumbi wa starehe au mikutano | 140,000 | kila kibali |
| 20. | Bwawa au Lambo | 40,000 | kwa kibali |
| 21. | Majengo mengine ambayo hayakutajwa | 40,000 | kwa kibali |
| 22. | Kibali cha kubomoa jengo | Asilimia hamsini (50%) ya ada ya kibali cha ujenzi | kwa kibali |
| 23. | Kibali cha ukarabati jengo | Asilimia ishirini (20%) ya ada ya kibali cha ujenzi | kwa kibali |
| 24. | Ada ya uhakiki wa umiliki kiwanja au shamba | 40,000 | Kila ombi |
| 25. | Ada ya ukaguzi wa ramani | 40,000 | Kila ombi |

*(a) Ada ya mabadiliko ya Matumizi (Alteration) ya jengo*

| *Namba* | *Aina ya Jengo* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Makazi kuwa biashara | 20,000/= | kila kibali |
| 2. | Makazi kuwa kiwanda | 25,000/= | kila kibali |
| 3. | Biashara kuwa kiwanda | 25,000/= | kila kibali |
| 4. | Makazi/biashara kuwa kituo cha mafuta | 30,000/= | kila kibali |
| 5. | Makazi/biashara kuwa bohari, ghala, kumbi za starehe | 50,000/= | kila kibali |

## SEHEMU YA SITA
## ADA YA WAKANDARASI NA UNUNUZI WA ZABUNI ZA HALMASHAURI

| *Namba* | *Aina ya Huduma* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya Wakandarasi | Asilimia mbili (2%) ya malipo | Kila Cheti |
| 2. | Ukusanyaji wa Mapato | 100,000/= | Kila zabuni |
| 3. | Ujenzi wa Majengo ya Halmashauri | 150,000/= | Kila zabuni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Ujenzi wa barabara | 150,000/= | Kila zabuni |
| 5. | Ukusanyaji na utupaji wa Taka ngumu | 50,000/= | Kila zabuni |
| 6. | Kupakua mashimo ya maji machafu (vyoo) | 70,000/= | Kila zabuni |
| 7. | Kurekebisha na kujenga vyoo vya uma, maduka na vioski | 80,000/= | Kila zabuni |
| 8. | Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo) | 100,000/= | Kila zabuni |
| 9. | Ukaguzi na upimaji wa viwanja | 100,000/= | Kila zabuni |
| 10. | Usimamizi na uendeshaji vyoo vya umma na maduka | 100,000/= | Kila zabuni |
| 11. | Huduma elekezi/mshauri (Consultancy services) | 100,000/= | Kila zabuni |

SEHEMU YA NANE

ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| *Namba* | *Aina ya Chombo cha usafiri* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Teksi | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | Gari ndogo aina ya Pick –up chini ya tani 3 | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Lori tani 3.5 hadi tani 7 | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Lori tani 7 na kuendelea | 80,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | Gari lolote la mizigo chini ya tani moja (1) | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Mabasi yanayobeba abiria chini ya 25 | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7. | Mabasi Makubwa zaidi ya abiria 25 | 70,000/= | Kwa mwaka |
| 8. | Pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda) | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 9. | Pikipiki za Magurudumu matatu (Bajaji na Guta) | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 10. | Trekta zinazofanya biashara | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 11. | Noah | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 12. | Gari lolote dogo lisilotajwa hapo juu | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 13. | Gari lolote kubwa lisilotajwa hapo juu | 30,000/= | Kwa mwaka |

SEHEMU YA TISA

USHURU WA MIFUGO

| *Namba* | *Aina* | *Kiwango (Shilingi)* | *Aina ya Mnyama* | *Idadi* |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo | 8,000/= | Ng'ombe, Punda na Farasi | Kila mnyama kwa siku |
| | | 3,500/= | kwa Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, Mbwa na wanyama wengine | Kila mnyama kwa siku |
| 2. | Ushuru wa Kununua Ngozi | 1,000/= | Ng'ombe | Kwa ngozi |
| | | 500/= | Mbuzi, Kondoo | Kwa ngozi |
| 3. | Cheti cha Afya cha usafirishaji wa Nyama na ngozi | 2,000/= | Ng'ombe, Punda na Farasi | kwa cheti kimoja |
| | | 1,000/= | kwa Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, Mbwa na wanyama wengine | kwa cheti kimoja |
| 4. | Kibali cha kusafirisha Nyama na Ngozi za wanyama | 2,000/= | Ng'ombe, Punda na Farasi | Kila kilo 10 za nyama na kipande kimoja cha Ngozi kwa kibali |
| | | 1,000/= | kwa Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, Mbwa na wanyama wengine | Kila kilo 5 za nyama na kipande kimoja cha Ngozi kwa kibali |
| 5. | Ushuru wa mifugo minadani | 5000/= | Kwa ng'ombe mmoja | Atakaeuzwa |
| | | 2000/= | Kwa mbuzi mmoja | Atakaeuzwa |
| | | 2000/= | Kwa kondoo mmoja | Atakaeuzwa |

## SEHEMU YA KUMI
## USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| *Namba.* | *Aina ya Zao* | *Kiasi cha Ushuru kwa mazao ya chakula (Shilingi)* | *Kiasi cha ushuru kwa mazao ya biashara (Shilingi)* |
|---|---|---|---|
| 1. | Viazi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 2. | Kabichi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 3. | Vitunguu | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 4. | Nyanya | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 5. | Nanasi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 6. | Nazi | 2% ya Bei ya | 3% ya Bei ya kununulia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kununulia | |
| 7. | Maharage | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 8. | Karanga | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 9. | Njugu | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 10. | Mbazi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 11. | Kunde | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 12. | Alizeti | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 13. | Mahindi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 14. | Ufuta | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 15. | Uwele | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 16. | Mtama | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 17. | Mpunga | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 18. | Muhogo | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 19. | Karoti | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 20. | Ndizi | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 21. | Matunda Mchanganyiko | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 22. | Mazao mengineyo yasiyotajwa hapo juu | 2% ya Bei ya kununulia | 3% ya Bei ya kununulia |
| 23. | Ada ya kibali cha kununua mazao ya biashara | 2% ya Bei ya kununulia | 40,000/= kwa tani |
| 24. | Ada ya kibali cha kununua mazao ya chakula | 2% ya Bei ya kununulia | 20,000/= kwa tani |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

ADA NA USHURU WA MAZAO YA MISITU

| *Namba* | *Aina Ya Zao La Misitu* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa: - | | |
| | (i) Mbao | 1,000/= | kwa ubao mmoja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (ii) Shata mlango au dirisha | 2,000/= | Kila moja |
| | (iii) Fremu mlango au dirisha | 1,000/= | Kila moja |
| | (iv) Kitanda | 5,000/= | Kila moja |
| | (v) Kabati | 5,000/= | Kila moja |
| | (vi) Kochi | 2,000/= | Kila moja |
| | (vii) Magogo | Asilimia 5% ya bei ya kuuza | |
| | (viii) Mirunda | 50/= | kwa mrunda mmoja |
| | (ix) Nguzo za simu | 2000/= | kwa nguzo moja |
| | (x) Nguzo za umeme | 5000/= | kwa nguzo moja |
| | (xi) Kuni | 3000/= | kwa tani |
| | (xii) Mkaa | 5000/= | kwa gunia moja |
| | (xiii) Mabanzi | 5000/= | kwa tani moja |
| | (xiv) Asali | Asilimia 5% ya bei ya kuuza | - |
| | (xv) Nta | Asilimia 5% ya bei ya kuuza | - |
| | (xvi) Ubuyu na Ukwaju | 150/= | Kwa kila debe moja |
| | (xvii) Mkeka, Kikapu na Ungo | 100/= | Kwa kila moja |
| | (xviii) Vinyago vya mpingo | 250/= | Kwa kila ki moja |
| | (xix) Vinyago vya miti mingine | 150/= | Kwa kila kimoja |
| | (xx) Mazao mengine ya misitu | 5000/= | kwa tani moja |
| 2. | Ada ya Leseni ya uvunaji | Inategemea na Zao linalovunwa | |
| 3. | Ada ya Leseni ya Biashara ya Mazao ya Misitu | 200,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Ada ya Usajili wa kufanya biashara ya Mazao ya Misitu | 100,000/= | Kwa mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
USHURU MWINGINE

| *Namba* | *Aina* | *Kiwango (Shilingi)* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1. | Ada ya muhtasari wa Halmashauri | 2,000/= | Kila maombi |
| 2. | Ushuru wa vituo vya kuoshea magari na vyombo vingine vya usafirishaji | 4,000/= | Kwa mwezi |
| 3. | Kibali cha kufyatua tofali za udongo (biashara) | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Ushuru wa chuma chakavu | | |
| | (a) Tani 1 | 6,000/= | Kila inaposafirishwa |
| | (a) ½ Tani | 3,000/= | Kila inaposafirishwa |
| | (b) ¼ Tani | 2,000/= | Kila inaposafirishwa |
| 5. | Kibali cha kuuza pombe za Kienyeji | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Kibali cha kutengeneza pombe za Kienyeji | 5,000/= | Kwa kila kibali |
| 7. | Ushuru wa vilabu vya pombe | 20,000/= | Kwa mwaka |
| | *Ushuru* | *Biashara Kuu* | *Tawi* |
| 17 | Wakala wa pombe za viwandani | 100,000/= Kwa mwaka | 80,000/= Kwa mwaka |
| 18 | Visima vya maji vya biashara au vituo vya kuuzia maji | 30,000/= Kwa mwaka | 30,000/= Kwa mwaka |

USHURU WA MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO KWENYE HIFADHI YA BARABARA

| Aina ya chombo na uzito | Kiwango cha ada ya maegesho kwa saa (Shilingi) | Kiwango cha ada ya maegesho kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| Gari uzito usiozidi tani moja na nusu | 200 | 500 |
| Gari uzito unaozidi tani moja na nusu na usiozidi tani tatu | 300 | 1000 |

*Tangazo la Serikali Na. 510 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| Gari uzito unaizidi tani tatu na usiozidi tani 10 | 500 | 1500 |
| Gari uzito unaozidi tani kumi na usiozidi tani 35 | 1000 | 5000 |
| Pikipiki za magurudumu matatu na nyinginezo | | 200 |
| Pikipiki (boda boda) | | 200 |

NB: Viwango vya ada katika megesho maalum ni Tsh. 3,000/= meta moja ya mraba kwa mwezi.

*(b) Ada ya Mashamba Makubwa*

| *Namba* | *Ukubwa wa shamba* | *Kiwango (Shilingi)* | *Muda* |
|---|---|---|---|
| 1. | Ekari Moja (Skimu ya Umwagiliaji) | 500,00 | Kwa mwaka |
| 2. | Ekari Kumi na kuendelea (Nyanda Kame) | 500,00 | Kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 12)*

FOMU YA KUFIFILISHA MAKOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ya Mwaka 2024.

Na kwamba niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa mahakamani.
Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe…………. ya mwezi…………..… mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..……………………......
Saini………………………..……………………………..………

Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro imegongwa kwenye Sheria ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro uliofanyika tarehe 27 mwezi 10 Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya;

GRACIAN MAX MAKOTA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro*

BARAKA KANUNGA LAIZER
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
13 Mei, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais*
*(Tawala za mikoa na serikali za mitaa*)